



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI MAFINGA



Uripaji wa taratibu taja:

Kumb. Na. MTC/20141

20/10/2025

Kamishna wa Ardhi Msaidizi,

Mkoa wa Iringa.

S. L. P. 785,

IRINGA.

**YAH: KUWASILISHA FOMU NA. 1 YA UWEKEZAJI KWA
KIWANJA NA. 2 KITALU 'F' LUGANGA
HALMASHAURI YA MJI MAFINGA**


Kichwa cha barua hapo juu chahusika.

2. Eneo linapopatikana viwanja tajwa, lilikuwa linamilikiwa kiasili na ndugu **ALFONSI SINGONDAMA NYAKUNGA**, ambaye aliliuza kwa kampuni ya **HUAFEI COMPANY LIMITED**, kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni Tanzania kama kampuni ya Kigeni (*Foreign Company*) likiwa na ukubwa wa mita za mraba thelathini na saba elfu mia nane sitini na mbili (37,862 sqm).

3. Kampuni ya **HUAFEI COMPANY LIMITED** mara baada ya kununua eneo hili, walifanya upangaji na upimaji wa eneo na kutoka kiwanja tajwa kwa matumizi ya kiwanda. Kwa kuwa kampuni hii ni kampuni ya kigeni ambayo kwa mujibu wa sheria, inatakiwa kumiliki ardhi kwa ajili ya uwekezaji (*under derivative Rights*), hivyo basi nimeandaa fomu ya ardhi namba moja inayotambua utengwaji wa ardhi hiyo kwa ajili ya uwekezaji (*designation of land for investment purpose*) ili imilikishwe kwa *Tanzania Investment and Special Economic Zones Authority* kama taratibu zinavyoelekeza.

4. Pamoja na barua hii, ninaambatanisha mkataba wa mauziano wa shamba kati ya **Alfonsi Singondama Nyakunga** na **Huafei Company Limited**, *Certificate of Incorporation, Memorandum and Articles of Association, Certificate of Incentives, official search ya Brela, Pasi za kusafiria za Wakurugenzi wa kampuni, Certificate of Capital Gain Tax*, na ramani ya upimaji wa viwanja kwa hatua zaidi.

5. Naomba kuwasilisha.


Geoffrey E. Kabuje

AFISA ARDHI MTEULE

HALMASHAURI YA MJI MAFINGA

**APPROVED OFFICER
MAFINGA TOWN COUNCIL**

Nakala kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Mji Mafinga,
S. L. P. 96,- **MAFINGA.**